**TANGAZO KWA UMMA**

Katika kutekeleza Ahadi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa shilingi Bilioni 200 kwa vijana ndani ya siku 100 baada ya kuingia madarakani kwa ajili ya kufanya biashara ndogo, za kati na kampuni changa. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana (OR - MV), Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI), na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inatangaza fursa ya mikopo nafuu kwa vijana ili kupata mitaji na kujiajiri. Mikopo inalenga kutoa vifaa na pembejeo za ufugaji wa samaki kwa vizimba (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa), zana za uvuvi, ufugaji wa kuku, ufugaji wa nguruwe, ufugaji wa mbuzi na kondoo, miundombinu ya ubaridi, na uchakataji wa dagaa na mwani. Vigezo na maelekezo kwa waombaji: -

i. Kuwasilisha barua ya maombi na fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu;
ii. Mkazi wa eneo husika na barua ya uthibitisho kutoka kwa Mtendaji wa Serikali za Mitaa/Vijiji;
iii. Raia wa Tanzania;
iv. Kijana (umri wa miaka 18 hadi 35) akiwa yeye binafsi au katika kampuni ya vijana, chama cha ushirika cha vijana, au kikundi cha vijana kilichosajiliwa na Halmashauri husika;
v. Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) kwa kampuni;
vi. Awe na barua na vitambulisho (NIDA) vya wadhamini wawili (2) wanaotambulika kwenye uongozi wa Serikali ambao watawajibika kulipa deni endapo mnufaika atakiuka masharti ya mkopo huu;
vii. Awe na akaunti ya benki na namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mnufaika;
viii. Awe na andiko la mradi lenye maelezo ya kwanini anahitaji mradi husika (isizidi kurasa mbili);
ix. Awe na rekodi nzuri ya urejeshaji wa mikopo katika taasisi za fedha;
x. Asiwe kwenye ajira rasmi au nia ya dhati ya kuajiriwa;
xi. Awe na nia ya dhati ya kujiajiri kupitia mradi huo;

Vijana ambao wapo tayari kukopa wawasilishe maombi yao katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kabla au ifikapo tarehe 03 Aprili, 2026. Fomu ya maombi imeambatishwa.

Imetolewa na:

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**
**S.L.P 2847**
**40487 DODOMA**
**Simu: +255 26 23 22613**
**Barua pepe: ps@mlf.go.tz**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Affix recent coloured passport size photograph

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**FOMU KWA AJILI YA MAOMBI YA MIKOPO YA VIJANA KUPITIA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

## 1.0. MAELEZO

Fomu hii itajazwa na mwombaji binafsi au kiongozi wa kampuni, kikundi, au chama cha ushirika cha vijana kinachoomba Mkopo. Viambatisho vifuatavyo ni muhimu kwa ajili ya uhakiki wa mwombaji wa mkopo:

i. Barua ya maombi
ii. Barua ya Utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji Kata (Igongwe muhuri)
iii. Udhibitisho wa uraia wa Tanzania (kitambulisho cha taifa - NIDA au Namba ya NIDA au kadi ya mpiga kura au cheti cha kuzaliwa au hati ya kusafiria);
iv. Cheti cha usajili wa kikundi, chama cha ushirika au kampuni;
v. Nakala ya Katiba ya Kikundi au Chama cha ushirika au Hati ya makubaliano na kanuni za kampuni;
vi. Wasifu (CV) ya mnufaika au viongozi wa kikundi, chama cha ushirika au kampuni;
vii. Cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN) kwa kampuni;
viii. Barua na vitambulisho (NIDA) vya wadhamini wawili (2) wanaotambulika kwenye uongozi wa Serikali ambao watawajibika kulipa deni endapo mnufaika atakiuka masharti ya mkopo huu;
ix. Uthibitisho wa akaunti ya benki na namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mnufaika na
x. Andiko la mradi lenye maelezo ya kwanini anahitaji mradi husika (isizidi kurasa mbili).

## 2.0. Taarifa ya kikundi

i. Jina la mwombaji ……………………………;
ii. Aina ya Mwombaji (Binafsi/kikundi/Chama /Kampuni)…………………………
iii. Majina ya Viongozi (kikundi/Chama /Kampuni) na namba za simu
   - ✓ M/Kiti: Jina…………………………....... Simu.............................................
   - ✓ Katibu: Jina…......................................Simu ........................................
   - ✓ Mhazini (vikundi na vyama vya ushirika)/Mhasibu (Kampuni):
     Jina ...................................... Simu........................................

iv. Idadi ya wanachama (kikundi/Chama /Kampuni)………Ke………Me………….
v. Anwani Kamili ......................................................................................

## 5.0 KWA AJILI YA MATUMIZI YA OFISI TU

Baada ya tathmini ya maombi kubaini kama mwombaji anastahili/hastahili kupewa mkopo

A. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Halmashauri/Jiji/Mji/Manispaa/Wilaya
Jina la Afisa…………………………...…Cheo……………

Halmashauri ya …………………………. Sahihi………………… Tarehe…………...

Anastahili/hastahili kupewa mkopo:

Maoni/sababu ya maamuzi hayo:……………………….....................……………
……...........................................................................................................................

B. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa.
Jina la Afisa………………………………………………Cheo…………………………
Mkoa ……………………………. Sahihi……………………… Tarehe………….
Anastahili/hastahili kupewa mkopo:

Maoni/sababu ya maamuzi hayo:……………………….....................……………
……...........................................................................................................................

C. Sehemu hii itajazwa na Afisa aliyeidhinishwa kutoka Ofisi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi
Jina…………………………………Cheo………………………………………….
Idara…………………………………Sahihi…………………. Tarehe………………….

Maoni……………………………...............…………………………………………